

# Zara & Mika

## Kuongoza Mabadiliko Chanya Katika Jamii Zao

*Rehman Kasule*



Kilitengenezwa kwa  
Kushirikiana na:



# Zara & Mika

Kuongoza Mabadiliko  
Chanya Katika Jamii Zao

*Rehman Kasule*

© Haki miliki 2021 - Haki zote zimehifadhiwa.

ISBN – 978-9913-9930-0-5

Maud yaliyomo ndani ya kitabu hiki hayawezi kuzalishwa tena, kunakiliwa au kusambazwa bila ruhusa iliyoandikwa moja kwa moja kutoka kwa mwandishi au mchapishaji.

Hakuna katika hali yoyote, lawama yoyote au wajibu wa kisheria utakaochukuliwa dhidi ya mchapishaji, au mwandishi, kwa uharibifu wowote, fidia, au upotezaji wa fedha kutokana na habari zilizomo ndani ya kitabu hiki, ama moja kwa moja au kwa njia isiyo ya moja kwa moja.

#### **Ilani ya Kisheria:**

Kitabu hiki kimelindwa kwa haki miliki. Ni cha kutumiwa na mtu binafsi pekee. Huwezi kurekebisha, kusambaza, kuuza, kutumia, kunukuu sehemu yoyote, au maudhui ndani ya kitabu hiki, bila idhini ya Rehmah Kasule au Mastercard Foundation.

#### **Ilani ya Kanusho:**

Tafadhali kumbuka habari zilizomo ndani ya hati hii ni kwa madhumuni ya elimu na burudani tu. Jitihada zote zimetokelezwa kuwasilisha habari sahihi, hadi sasa, za kuaminika, na kamili. Hakuna dhamana ya aina yoyote iliyotangazwa au kudokezwa. Wasomaji wanakubali kwamba mwandishi hashiriki katika utoaji wa ushauri wa kisheria, kifedha, Kimatibabu au kitaaluma. Maudhui ndani ya kitabu hiki yametokana na vyanzo mbalimbali. Tafadhali wasiliana na mtaalamu mwenye leseni kabla ya kujaribu mbinu yoyote iliyotajwa katika kitabu hiki.

Kwa kusoma kitabu hiki, msomaji anakubali kwamba katika hali yoyote mwandishi hawajibiki kwa hasara yoyote, moja kwa moja au isiyo ya moja kwa moja, ambayo ina patikana kwa sababu ya matumizi ya habari zilizomo ndani ya kitabu hiki, ikihusisha lakini isiyojikita kwenye makosa yaliyowachwa au yasiyo sahihi.

**Kimechapishwa na kupigwa chapa katika Jamhuri ya Uganda.**

## **Kujitolea**

Tunatoa kitabu hiki kwa watoto wote duniani kote. Tunatumai kwamba unapokisoma, utaweza kuhamasishwa na kuchukua hatua za kuyasimamia maisha yako na kuleta mabadiliko katika jamii yako. Dunia inahitaji kusikia hadithi zako za hofu, ujasiri, matumaini, na matarajio. sema; Sauti yako ni muhimu!

## **Shukrani – Uwezo Wetu**

Kuandika na kuchapisha kitabu huchukua ushirikiano. Nilipo kuwa na wazo zuri la kuandika kitabu hiki nilihitaji ushirikiano kuweza kulitimiza. Ninaishukuru timu iliyonitolea msaada mkubwa nilipokuwa nakishughulikia kazi hii. Shukrani za kibinafsi kwa timu ya wahariri na waandishi, Pheona Nakishero na Zura Nakiwoga Mukasa. Mbunifu wa picha na mchoraji, asante kwa kazi nzuri mlioifanya kwenye kitabu hiki na kuyawezesha mawazo yangu yakawa kweli. Pia nawatambua watoto wabunifu Asra, Amaal, na Rahma, ambao walimuunga mkono mwimbaji wetu nyota inayochipuka na mshairi Kauthar Lukwanzi.

Ninawashukuru daima watoto wote nchini waliotusimulia hadithi zao. Hadithi zao zili kuwa masomo ya ajabu yatakayowawezesha watoto wengine duniani kote kuwa wazuri. Ninawashukuru pia wazazi waliowahimiza watoto wao kuitikia wito wetu na kutusimlia hadithi zao. Shukrani kwenu nyote kwa ushirikiano wenu. Pia ninawashukuru wazazi waliowahimiza watoto wao kuitikia mwito wakushiriki kwa kueleza hadithi zao. Asanteni sana kwa ushirika wenu.

Kimefafanyiliwa na: Davis Bamwine

Kimeandaliwa na: Patricia Businge

## Kuhusu Mastercard Foundation

Mastercard Foundation inafanya kazi na mashirika ya maono ili kuwawezesha vijana katika Afrika na jamii asili za Canada kupata kazi yenye heshima na ya ukamilifu. Ni mojawapo ya mashirika makubwa ya kibinafsi ulimwenguni yaliyona malengo ya kuendeleza elimu na kutoa msaada wa kifedha ili kuunda ulimwengu ulio na usawa kwa wote. Mastercard Foundation ilianzishwa mwaka wa 2006 kama shirika huru na kamati ya Wakurugenzi na usimamizi.

Mastercard Foundation inatekeleza Kampeni ya kufahamisha Umma kuhusu athari za KOVID-19 kwa watu binafsi, familia na jamii zilpojitokeza zaidi barani Afrika katika mwaka wa 2021. Kampeni hiyo, iliyotekelezwa nchini Ghana, Kenya, Nigeria, Uganda, Senegal, Rwanda, na Ethiopia, inawapa vijana nafasi kusimulia visa vya ustahimilivu, ubunifu na kujitolea kwa kuitikia mwito mpana wa KOVID-19.

Shughuli hizo zimejikita katika kauli mbiu ya Jilinde, Linda familia yako, Linda jamii, zikisisitiza haja ya uwajibikaji wa kibinafsi chini ya alama ya reli #nijuuyetusisi

Kwa habari zaidi kuhusu MasterCard Foundation, tafadhali tembelea <https://mastercardfdn.org/>; na kujifunza zaidi kuhusu ujasiri wa vijana kote bara wakati wa janga, tafadhali tembelea: [www.covidhqafrika.com](http://www.covidhqafrika.com)



## Ujumbe kutoka kwa Mwandishi

### Rehmah Kasule

Watoto wapendwa,

Baba yangu alifariki nilipokuwa mdogo, na maisha yalikuwa magumu sana, lakini familia yangu haikukata tamaa! Mama yangu aliungiza umuhimu wa elimu ndani ya bongo zetu. Nilizaliwa kijiji kama baadhi yenu, lakini sikuwa mwanamke wa kijiji kwa sababu nilielimika.

Katika shule yangu kijijini, hatukuwa na vitabu. Nilipojiunga na shule ya sekondari, rafiki zangu waliniingiza kwenye ulimwengu wa vitabu, na maisha yangu yakabadilika daima! Kwa kusoma vitabu, nilipata maarifa, nikajiamini, nikaanza kuwa na maono ya ajabu, nikaanza kuwa na matumaini ndani yangu. Nilitia bidii masomoni nikahitimu na shahada ya gredi ya kwanza katika chuo kikuu.

Nilikuwa na umri wa miaka 24 tu nilipoanza yangu kuunganisha wafanyabiashara na wateja na baadaye nikaanzisha shirika langu binafsi liitwalo CEDA International. Ninawafunza watoto kama wewe kujigundua wao ni nani, kujivunia wanakotoka, na kuwa na maono kuhusu ni wapi wangependa kuenda. Pia ninawasaidia watoto kupata elimu bora ya kuwawezesha kuwa viongozi na wajasirimali wa kesho.

Kila siku, ninawakumbusha binti zangu wawili kwamba unapokuwa na maono, unafanikiwa na hakuna ndoto yoyote ambayo ni kubwa sana. Ndoto yangu ya utotoni ilikuwa kusomea katika chuo kikuu cha Harvard nchini Marekani. Miaka michache iliyopita, nilitimiza ndoto hiyo nilipoitwa kuenda kusomea huko, nikishiriki kwa miaka miwili katika mpango wa uongozi wa juu kwa kuzingatia elimu ya kesho na kazi barani Afrika.

Sasa, nimeleta mambo mapya za Kiafrika kuwawezesha watoto kusimulia hadithi zao kupitia kwenye vitabu kama hivi. Nimedhamiria kuwasaidia watoto kujifunza kusoma. Ninaamini kwamba wasomaji ni viongozi!

Ushauri wangu kwa watoto kila mahali ni kwamba "Historia yako haiamui hatima yako; Unaweza kubadilisha maisha yako ya kesho unapojiamini na kukuza mtazamo wa imani."

*Rehmah Kasule*

**Rehmah Kasule**



## Athari za Ugonjwa wa KOVID-19

Janga la KOVID-19 au 'Corona Virus' ni virusi hatari vya homa, ambavyo vilianza Desemba 2019 nchini China, na kuenea ulimwenguni kote. Familia na jamii zilikabiliwa na hali ya kutofahamika wakati wa janga hili. Wakati ambapo watoto hawakuzingatiwa kuwa katika hatari kubwa ya kuambukizwa KOVID-19, wameathirika sana na janga hili katika nchi nyingi za Afrika.

Nchini Uganda mataifa mengine barani Afrika, watoto walio chini ya miaka 14 ni takribani asilimia sitini na tano ya idadi ya watu, na tangu janga hili lianze, shule zote zilifungwa kumaliza mwaka mmoja au miwili. Shirika la "Save the Children" linakadiria kuwa karibu watoto milioni tano hawakuweza kurudi shuleni baada ya janga hili. Benki kuu ya ulimwengu iliripoti kwamba janga lilizidisha hali ya ufukara na mahangaiko yaliyozidi kuenea katika jamii ilipanua bonde kati ya watoto. Watoto wengi shuleni hawafunzwi kwa sababu hawana ujuzi wa kimsingi wa kusoma. Hali ilikuwa mbaya zaidi kwa watoto walio katika mazingira tata kama makao ya wakimbizi na wale walio katika jamii za kipato cha chini. Watoto hawakuwa na vifaa vya kusoma na kujifunza na hakukuwa na zana za kuwasaidia kukabiliana na janga hili na kushiriki katika uzoefu wao wa msaada wa kihisia. Maudhui madogo yaliyopatikana hayakuzungumzia watoto, kuonyesha hali halisi ya maisha yao, wala kuwakilisha sauti zao. Hali hii ilikaribia Kubadilika!

### Kanuni za kuendeleza hali ya kujikinga (SOPs)



Vaa barakoa



Na maji safi



2m



Kaa mita mbili mbali na mwenzako

## Kuhusu Kitabu Hiki

'Sauti ya Watoto' ni kitabu cha mkusanyiko wa hadithi kutoka kwa watoto nchini Uganda wakieleza mapitio yao, na uzoefu wa maisha wakati wa janga hili la KOVID-19. Kitabu kinakuchukua kupitia safari, kikigusia vyakula, maliasili, maisha ya kila siku, na tamaduni ambazo hufanya Uganda kuwa na umahiri hata wakati wa shida. Kupitia usimulizi, kitabu hiki kinatoa habari muhimu ya kuzuia KOVID-19. Kinawapa watoto uwezo kukabiliana na kufaulu athari za janga hili.

Watoto watajifunza kutokana na hadithi za watoto wengine za ujasiri, tumaini, udadisi, utendaji, na moyo wa ujasiriamali. Kitabu hiki kinaendeleza mafunzo kwa kupitia uigizaji, (elimu ya kutumbuiza). Kinawahimiza watoto wainue paze sauti zao. Kinawawezesha kupata vifaa halisi na ufahamu wa kuwaweka katika hali ya imani na kuelimika.

Kitabu hiki kinajumuisha shughuli za kujifunza ambazo zitakushirikisha katika kutumia kujithamini, kutafakari, mawazo muhimu, na ujuzi wa kutatua shida ili kujenga ujasiri wa kukabiliana, kuishi, na kustawi. Kitabu cha Sauti ya watoto kinalenga kuwawezesha watoto wa umri wa miaka 9-13 kufahamu na kushiriki katika shughuli za kubadilisha jamii. Kitabu kinawahimiza kuyatawala maisha yao ili wabadilisha jamii zao.

Suti ya watoto ilitekelezwa kwa kushirikiana na Mastercard Foundation ili kuendeleza masomo kama mojawapo ya njia kampeni ya kuleta kulewa kuhusu janga la KOVID-19 katika mwaka wa 2021. Shirika linashughulikia maandalizi ya utaratibu wa masomo nchini Uganda (NCDC) lilikipa idhini kitabu cha Sauti ya watoto kuwahimiza na kushirikisha watoto katika shule za msingi kuzindua kuoma kwa awali. Watu wanaweza kupata kitabu hiki katika pdf, vifaa vya sauti, "flipbook" na kwa uigizaji katika lugha zaidi ya saba. Unaweza pia kutembelea [www.rehmahkasule.com](http://www.rehmahkasule.com)



# YALIYOMO

## Mada ya kwanza

### Kila dhoruba Hupita

Mwangaza wa jua huleta mwale wa tumaini

## Mada ya pili

### Shukrani na Upashaji

Kurudi pamoja na familia katika jamii

## Mada ya tatu

### Kutambua Wewe ni nani

Uhakika wa mimi ni nani

## Mada ya nne

### Ongea, Sautiyako Ni Muhimu

Jifunze vifaa vipya ushinde hofu

## Mada ya tano

### Huruma Hupunguza Shutuma

Kujadiliana na kujifunza visa vya watoto vya ustahimilivu

## Mada ya sifa

### Vitu chanya Vinavyotuzingira

Watoto wanajitahidi masomoni

## Mada ya saba

### Tumaini la siku za mbeleni

Kuelekeza mawazo kufanya tumaini liwe la kutimika

## Mada ya nane

### Nguvu Zetu – Pamoja ni Wenye Nguvu

Kuunda hali ya siku zijazo iwe ambayo tunatarajia kuona

## Mada ya tisa

### Inuka na Uangaze

Kupewa zawadi na kutambulika bungeni na kwenye umoja wa mataifa ya ulimwengu

## Mada ya kumi

### Kuwa na la kufanya – ni juu yetu

Watoto wanaahidi kuleta mabadiliko

## Hadithi za Watoto

Matumaini, Ujasiri, Shukrani, Uthabiti, Kuchua hatua na Ujasiriamali kutokana na watoto wa Uganda

### Shughuli, Michezo, Wimbo na Shairi

Kitabu hiki kinatuzwa kwa

“**Historia yako haiamui hatima yako. Unaweza kubadilisha maisha yako ya kesho unapojiamini na kukuza mtazamo wa imani.**”

Rehmah Kasule




# Kila Dhoruba Hupita

## Mwangaza wa jua huleta mwale wa tumaini

Ilikuwa Ijumaa, mchana. Harufu, tamu ya ndizi na samaki iliyochoywa katika urojo wa njugu ilienea jikoni katika nyumba ya familia ya Kego, walipoket kula chakula cha mchana. Harufu nzuri ikaelea nje kupitia kwenye dirisha la jikoni hadi mtaani Nkumba katika kitongoji cha Entebbe nchini Uganda.

"Hiki ni chakula ninacho kipenda kuliko vingine daima! Naweza kukila Kila siku" Mika mwenye umri wa miaka kumi na mmoja alisema akiuramba urojo uliokuwa kwa sahani yake.

"Ni hicho tu unachopika tangu ulipojifunza kupika. Mika ninaweza kupika 'luwombo' tamu kuliko wewe," Zara akasema. Yeye ni mdogo wa Mika kwa mwaka mmoja tu, na siku zote wanashindana.



Bi Kego alitabasamu akiwaangalia watoto wake. "Tazama, mama anakubaliana nami. Anapenda urojo wangu," Mika akajivuna.

"Ni kweli hivyo, na urojo huu ni unafaa kwa afya yangu," Bi Kego akasema.

Walikatizwa na mlipuko wa radi, na mvua ikaanza kunyesha na kugonga juu ya paa lao la chuma. Matone makubwa ya maji yalidondoka chini kwenye baraza ya nyuma.

"Baba yenu itamlazimu kurekebisha paa hili linalovuja atakaporudi nyumbani," Bi Kego akasema, huku akikosa pumzi anapongea.

"Mama, uko sawa? Je, wewe ni mgonjwa tena?" Mika akauliza, kwa hofu.


"Mimi si mgonjwa tena," Bi Kego akasema, "lakini nitachukua muda kabla ya kujihisi vizuri kama kawaida tena."

Bi Kego aliambukizwa KOVID-19 wiki chache zilizopita. Hata hivyo, alipona kutokana na ugonjwa huo, alikuwa angali udhaifu. Daktari alimshauri kufanya mazoezi ya matembezi na kukaa juani kila asubuhi ili kumsaidia kusimama vyema tena.

Mvua ilipungua na kubaki manyunyu tu huku jua likiangaza kupitia matone ya mvua.

"Ajuza alikua akisema kwamba jua hili hutokea wakati simba anapojifungua!" Susan mwenye umri wa miaka saba alisema akichungulia dirishani. "Je, tunaweza kwenda nje tukafanya mazoezi ya kutembea Mama?"

"Baada ya kuosha vyombo, sote tunaweza kwenda nje na kupata jua," Bi Kego akajibu.



Baada ya dakika chache, watoto na mama yao wakatembea kupitia mlango wa nyuma ya nyumba yao yenye matofali mekundu. Wakatembea hadi kwenye mti mkubwa wa maembe ulioko uani. Watoto wakafurahia kuwa nje wakiota jua. Susan akavuta kitambaa cha kichwa cha Zara kwa utani, na wakaanza kukimbia.

Kwa mbali, Mika akawaona watoto wengine wakicheza uwanjani.

"Kwa kweli natamani kucheza kandanda na marafiki zangu," akasema.

Tangu kufungwa kwa siku 42 kwa siku za COVID-19 kulikowekwa na serikali, watoto hawakuwahi kutoka nyumbani.

"Najua lakini kukaa nyumbani kunasaidia kuzuia kuambukizwa na kuenea kwa COVID-19," Bi Kego akasema.

"Je, tunaweza kucheza michezo bila kukaribiana na huku tukiwa tumevaa barakoa?" Susan akauliza.

"La hash! Sijawahi kuona mtu akicheza kandanda akiwa amevaa barakoa," Mika akasema.

"Labda tunaweza chezea nyumbani," Bi Kego akasema.

"Ni wazi timu yangu itashinda," Mika akajigamba.

"Tutaona," Zara akamjibu.

Ingawa Zara hakupenda mchezo wa kandanda, hakushiriki mchezoni. Alikubaliana na Bi Kego dhidi ya Susan na Mika.

Mchezo huu ni wa kushindana. Zara alifunga bao la kwanza, akakimbia na kupiga chenga, haraka, akafunga bao la pili.

"Mama, nina kazi tuliyopewa shuleni ya kufanya," Susan akasema kabla ya mechi kuanza tena.

"Ni kwa sababu timu yako inapoteza?" Zara akasema.


Bi Kego akacheka, "Hapana, hebu tuingie ndani. Zoezi hilo limenitosha.

"Mama, je, Zara na mimi tunaweza kuwa na matembezi barabarani?" Mika akamwomba mama yake. "Tutawaamkua marafiki zetu kwa umbali.

"Tutavaa barakoa zetu wakati wote," Zara akasema, akiondoa moja kutoka mfukoni mwa vazi lake la rangi ya bluu.

"Najua nyinyi ni watoto wanoajibika Lakini muwe waangalifu na kumbukeni kunawa mikono yenu mnaporudi. Shikeni hela hizi tafadhali, mtanunua matunda mtakaporudi nyumbani," Bi Kego akasema, huku akimpa Mika shiling elfu tano.





Punde Zara na Mika wakatoka nyumbani. Njiani, waliona bustani iliyojaa maua ya yanayong'aa. Kuna maua marefu ya waridi, nyeupe, fupi, zambarau, kubwa naya manjano, yote katika bustani hii.

"Ee! Tumpelekee Mama baadhi ya maua haya, yaliyo nyumbani yamenyauka." Mika akasema.

Wakainama na kukusanya maua machache, wakayapanga na kuyafunga katika shada moja linalopendeza.




# Shukrani na Upashaji

## Kurudi pamoja na familia katika jamii

Mika na Zara kwa walivuka daraja dogo kwa uangalifu linaloelekea kwenye uwanja wa michezo. Huko, walikutana na rafiki zake Mika kutoka shuleni- Alice, Abdu, na Justin. Waligusana viwiko kwa kusalamiana, vile walivyo shauriwa na wazazi wao pamoja na walimu kufanya hivyo tangu mwanzo wa janga la KOVID-19.

"Je, unataka kujiunga nasi, Mika?" Justin akauliza.

"Ndiyo!" Mika akasema kwa furaha.



Walikuwa hawajaonana na marafiki wao kwa muda mrefu. Wakati mama yake alipoambukizwa virusi vya korona, hawakuruhusiwa kutoka nyumbani.

Kila mtu alikuwa mwangalifu. Ni furaha hatimaye kutoka nyumani na kucheza na marafiki.

"Huyu msichana mdogo mrembo ni nani?" Alice akauliza.

Alice ana umri wa miaka kumi, kama Zara, na anapenda kupata marafiki wapya. Alice amesuka nywele zake.

"Huyu ni binamu yangu Zara," Mika akasema. "Mjomba wangu na mkewe, yani wazazi wake walipofariki, wazazi wangu walimleta Zara nyumbani kwetu baada ya mazishi yao."

"Ndiyo, nakumbuka. Ninasikitika sana Zara," Alice akasema.

"Asalam Aleikum, Zara," Abdu akamsalimia.

"Walaikum Salaam," Zara akajibu.

Baada ya kuwaeleza kuhusu Zara, Mika akauliza marafiki zake walichokuwa wakifanya wakati huo ambao shule zilipokuwa zimefungwa.

"Hakuna mengi, wakati mwingine nahisi huzuni" Alice akasema. Wazazi wake hawakuweza kulipia gharama za masomo ya mtandaoni.

"Si wewe peke yako," Zara akasema. "Niliona kwenye televisheni kwamba mamilioni ya watoto barani Afrika wamekuwa nje ya shule tangu janga hilo lilipoanza. Baadhi ya watoto, hasa wale walio katika kambi za wakimbizi na maeneo ya vijijini, hawana vifaa vya kusoma."

"Nina furaha kwamba shule zitafunguliwa mwezi ujao," Mika akasema.

"Ndiyo," Alice akakubali. "Sasa sina haja ya kuwa na wasiwasi juu ya kurudi katika darasa la sita mwaka ujao, lakini niko nyuma katika kazi za shule."

"Nina wazo!" Mika akamwambia. "Tunapata masomo kutoka kwenye madarasa yetu ya mtandaoni. Nitamuomba mama azichapishe ili tuweze kushiriki na Abdu na Alice kupata kazi za shule."

"Eee! itakuwa vizuri sana," Alice akasema, "Asante, tunashukuru sana, Mika."

Zara alifikiria, kisha akatamka, "Ndiyo! Hebu tucheze mchezo wa shukrani!"

"Ni aina gani ya mchezo huo?" Abdu akauliza.


"Shangazi yangu Madina alinifunza wakati wazazi wangu walipokuwa wagonjwa," Zara akajibu. "Kila siku una andika mambo kumi unayoshukuru katika kitabu."

"Lakini hatuna vitabu hapa," Abdu akasema.

"Nitakimbia na kuleta karatasi na kalamu kutoka nyumbani. Nyumba yangu iko hapo tu," Justin anajitolea.

Alikimbia nyumbani na kurudi na karatasi na kalamu. Watoto walikaa kwa duara nyanzi na kuunda orodha zao za shukurani. Kisha wakasoma orodha zao kwa sauti kubwa.

Kila mtu akashukuru juu ya familia, marafiki, chakula, maisha na afya yake.





# Kujua Wewe ni nani

## The Who am I self-affirmation

Mika alisimama kama miale ya mwangaza. "Hili linanikumbusha swali muhimu."

"Sasa ni nini, Mika? Natumai siyo hadithi zako za kijinga tena!" Zara akatania.

"La, la. Hebu fikiria kuhusu hilo kwa dakika. *Mimi ni nani?*" Mika akawaalika marafiki zake kutafakari pamoja naye. Tulumia muda kutafakari juu ya swali hili wakati wa mpango wa ushauri kwa viranja shuleni: *Mimi ni nani?*" Mika akaeleza.

"Hii ni dhahiri! Mimi ni mvulana," Abdu akasema.

Zara akatabasamu. "Wewe ni zaidi ya mvulana tu. Ndoto zako, shauku, na mahali unapotoka pia ni sehemu kubwa ya wewe ni nani."

"Ndiyo, mshauri wetu alisema kwamba ikiwa unajua wewe ni nani, unapata unachotaka," Mika akaongeza.

Zara akamtaka Mika kushiriki katika zoezi walilofanya kila asubuhi walipoamka. Kila mtu akamtazama Mika kwa mwongozo aliyokuwa akiashiria "**MIMI NI NANI?**" kujithibitisha mwenyewe. Mika akaeleza kwamba unapaswa ujitazame kwenye kioo na ujiulize swali hili.

"Sema kwa nguvu jinsi unavyoshangilia mchezo wa kandanda," Mika akasema. Hebu jaribu!" Zara akaruka. "Kwa hivyo, ninapouliza mimi ni nani, nyote mnajibu," Mika akawaongoza.



"Mimi ni nani?" akauliza Mika.

"Mimi ni nyota," wakajibu pamoja.

"Mimi ni nani?"

"Mimi ni bingwa."

"Mimi ni nani?"

"Mimi ni kiongozi."

"Mimi ni nani?"

"Mimi ni mshindi."

"Mimi ni nani?"

"Mimi ni mtoto mwerevu wa Kiafrika."

Wakacheka kwa msimko na kuinua mikono yao kwa kukunja ngumi.


"Unapokuwa unajiamini, hakuna kinachoweza kukuweka chini," Mika akawaambia.



VAA BARAKOA  
UKIWA MAHALI  
PA UMMA

Kwa mbali, Susan alikimbia kutoka nyumbani kuelekea waliko. Alipokariabia, shanga katika nywele zake ndefu zilizo sukwa zikafanya sauti—kilingi, kilingi, kilingi. Anakosa pumzi, lakini anaendelea kuruka juu na chini huku akipiga kelele.

"Mika na Zara, mama amesema ni wakati wa kurudi nyumbani kusaidia katika kazi ya jikoni."



OSHA MIKONO  
YAKO KWA SABUNI  
NA MAJI YANAYO  
TIRIRIKA



"Kwaheri. Hii imekuwa siku ya kuchangamsha," Abdu akasema.

"Ndio, ninahisi bora zaidi kuliko nilipoamka asubuhi ya leo," Alice akasema.

Justin akawaaga na akakuchukua karatasi na penseli zilizobaki. "Jihadharini, nendeni salama, na kumbukeni—" Kabla Justin hajamaliza, wote wakapiga kelele, "Vaa barakoa yako, nawa mikono yako, na jitenge usimkaribie mtu yeyote katika jamii."





Walipokuwa wakerudi nyumbani, walipitia katika duka la Nnalongo. Lililo na karoti, limau, tangawizi, nanasi, mboga na matunda mengine mengi na mboga. Zara akaununua ndizi mbivu.

Bi. Kego alipokuwa mgonjwa, walikuwa wakimnunulia karoti, tangawizi, limao, na nanasi kutoka kwenye duka hili. Pia walinunua dawa aina nyingi kutoka katika maduka ya dawa na hospitali. Mmoja wa marafiki zake pia alinunua dawa ya kienyeji yani majani ya miti kwa ajili ya kujifukiza.

Ulikuwa wakati wa hofu katika familia. Kwa bahati nzuri, hakuna mtu mwingine aliyeambukizwa virusi hivyo. Walikuwa makini kwa kunawa mikono yao kila wakati, kuvaa barakoa, na kutokaribia mtu yeyote. Pia walifanya orodha ya zamu za kufanya kazi za nyumbani, ili Bi. Kego asaidiwe kwa kazi hizo.

Watoto waliangalia upande wa barabara, boda boda zilizokuwa zimebeba maabiria, ziliendeshwa kwa kasi na kuacha vumbi nyuma. Kila mtu aliharakisha mwendo wake ili saa moja alasiri- yani saa ya kafyu iwadie akiwa nyumbani.

Walipofika nyumbani, jua lilikuwa limeanza kuzama na Bi Kego alikuwa akiwaongojea nje ya nyumba. Kabla ya kuingia ndani ya nyumba, akaawaambia kunawa mikono yao kwenye mfereji wa nje.

"Tunapaswa kunawa mikono yetu kwa muda gani?" Susan akauliza.

"Kwa angalau dakika mbili," Zara akasema.

"Tunaweza kuimba wimbo wa alfabeti mara tano a, ba, cha, da, ili kupata muda sahihi," Mika akaongeza.

Baada ya kuosha mikono yao pamoja na ndizi, Zara akampa mama yao shada la maua. Bi. Kego akafurahia sana maua hayo. Akalichukua ua la waridi kutoka kwa shada lile na akaliweka katika nywele zake na akawaonyesha jinsi linavyofanana na rinda lake la rangi ya waridi.

Susan akaelekea jikoni kuziweka ndizi kwenye kikapu cha matunda.

"Shangazi, kuna kitu kilicho na harufu nzuri sana," Zara akatabasamu.

"Najua. Nimewatayarishia kitu spesheli. Sasa, nendeni mjitayarishe kwa chajio. Ogeni na mbadilishe nguo zenu," Bi. Kego akasema.





# Ongea, Sautiyako ni Muhimu

## Jifunze vifaa vipya ushinde hofu

Wakati wachajio, watoto walishangaa kuona aina nyingine mpya ya chakula mezani, mfano kama chapat iisio nzito na pana.

"Baba, chakula hiki ni cha aina gani?" Susan akauliza.

"Hii ni Injera kutoka Uhabeshi," Bwana Kego akajibu.

"Ni kitamu sana," Mika akasema.



"Je, mnaweza kukisia ni nini kingine Uhabeshi inachofahamika nacho?" Bwana Kego akawauliza.

"Najua! Kahawa!" Zara akajibu. "Kama ilivyo Uganda, kahawa ni mojawapo ya mazao makubwa ya kilimo nchini Uhabeshi."

"Vizuri sana, Zara," Bwana Kego akasema akitabasamu.

"Baba Mika, tuambie kuhusu siku yako ya kwanza kurudi kazini baada ya kifungo," Bi. Kego akasema. Mumewe akaeleza kwa sauti ya chini, kwamba biashara nyingi bado zimefungwa na kuna watu wachache mjini.

"Janga hili limeirudisha nyuma dunia, lakini limeimarisha familia yetu," akasema. "Tuna fursa ya kula chakula pamoja."

Kabla ya kwenda kitandani, Bwana Kego aliwakumbusha watoto kwamba virusi vya KOVID-19 bado vinaenea sana. Wanapokwenda shuleni, lazima kila wakati wavae barakoa zao.

"Lakini baba, walimu wakituambia tutoe barakoa zetu wakati wa kuzungumza tufanyeje?" Mika akauliza.

"Hilo ni kosa. Paza sauti yako unapozungumza. Waonyeshe kwamba, hata kwa barakoa, unaweza kuzungumza na ukasikika," Bwana Kego akasema.


"Tunapaswa kufanya mazoezi. Ninaweza hata kuimba kwa sauti nikiwa na barakoa, sikiliza?" Zara akasema na kisha akaanza kuimba wimbo.



"Naupenda wimbo huu. Unatukumbusha kukumbana na hofu zetu, liwe liwalo," Mika akasema.

"Umesema ukweli, Mika. Pia unatuhimiza kuendeleza ndoto zetu." Zara akaongeza, na kuanza kuimba kwa sauti kubwa.

Wote wakajiunga na Zara katika kuimba kabla ya kwenda kitandani.



"Mimi ni nyota inayokua,

Mimi ni mtu wa ajabu,

Naota, ndio naota,

Naota kwa sababu

Mimi ni nyota inayoinuka.

Nina ujasiri

Kupambana na hofu zangu,

Ninafikia nyota ili,

Kutambua nguvu, za ndoto zangu.

Unapoota, unaweza kufanikiwa,

Kugundua maana ya kuishi huru na kuinuka zaidi kuliko ulivyoota ndani.

Ndani ya kila moyo,

Kuna cheche za miujiza ambazo huwasha na

Kuangaza katika mawazo yako na kuyabadilisha kuwa makuu, kutambua nguvu za, ndoto zako."





# Huruma Hupunguza Shutumama

Kujadiliana na kujifunza visa vya watoto vya ustahimilivu

Baada ya miezi sita ya kifungo, Bwana Kego aliacha watoto katika Shule ya Msingi Kaboga mapema asubuhi. Kuna mabango yenye ilani kwenye lango la shule na kila mahali uani kuwakumbusha watu kuvaa barakoa, kunawa mikono, na kutokaribiana ili kuzuia kuenea kwa KOVID-19.



Siku ya kwanza shuleni ilikuwa baridi, lakini watoto walifurahi kurudi baada ya kifungo. Walisalimiana kwa hofu na kwa umbali au wakigongana kwa viwiko. Walipoanza mazoezi ya asubuhi, hawakukaribiana.

Baada ya kuimba wimbo wa shule na kusali, mwalimu Bi. Okwi, aliwakaribisha shuleni na kuwatolea maelezo ya kimsingi kuhusu KOVID-19 na jinsi ya kuwa salama. Aliwaambia kila mmoja aungane na rafiki yake. Wachukue chati na kuweka alama ya tiki kwenye visanduku vinavyofaa.

Rafiki wa dhati wa Susan, Mariam, hayupo, na hakuwa na mtu wa kuungana naye.

“Mwalimu, kwa nini Mariam hajafika shuleni leo?” Susan akauliza.

Mwalimu alieleza kwamba Mariam hatarudi shuleni. Familia ya Mariam iliathiriwa vibaya na KOVID-19. Kwani dada yake aliporudi kutoka shule ya bweni, hawakugundua kuwa alikuwa na virusi, kwa hivyo vilienea kwa watu wengi katika familia yake waliambukizwa, akiwemo baba yake, mama, na shangazi yake. Wengine walipona, lakini mama yake Mariam alifariki.

“Dada yake Mariam lazima anasikitika sana kwa kueneza virusi kwa familia yake,” Abdu anasema.

“Kuambukizwa KOVID-19 si jambo la kuaibikia, watu wanapomfanya mgonjwa asikitike, huo ni unyanyapaa,” Akwi anasema.

“Tunawezaje kuzuia unyanyapaa kwa wagonjwa wa KOVID-19?” Abdu anauliza.

“Kwa kusambaza ukweli kuhusu KOVID-19 badala ya hofu, na kwa kuwa na hisani na kuwapa msaada wagonjwa na familia zao,” Mwalimu Akwi akajibu.

Watoto walikimbia kwenda darasani. Katika darasa la Mika, mwalimu aliwauliza watoto kujadili jinsi KOVID-19 ulivyowaathiri.

Alice alikuwa wa kwanza. “Nilishuhudia mabadiliko nyumbani,” akasema. “Biashara ya baba yangu ilipofungwa, hatukuweza kupata chakula kizuri tena. Uhusiano wa wazazi wangu pia ulibadilika. Walikasirishana na kupigana kila muda.”

Mika aliinua mkono wake na kuongezea, “Nilitazama habari kwenye runinga kwamba, katika nchi nyingine ambazo shule zilikuwa zimefungwa, baadhi ya watoto walidhulumiswa nyumbani.”

“Ndiyo, dhuluma za nyumbani zilikuwa kwa kiwanga cha juu wakati wa kifungo,” mwalimu akakubaliana naye.

Mwalimu alieleza kwamba wazazi wanapaswa kuajibika. Baadhi ya wazazi walifungwa gerezani, lakini watoto wengine hawakuweza wakamwambia mtu yeyote kwa sababu waliogopa.

“Nijambo la kusikitisha sana. Watoto wanapaswa kusema!” Zara akasema.

“Nina wazo. Tunahitaji kusaidiana kwa kupatiana mawaidha waweze kuwa na ujasiri zaidi na ustahimilivu.”

“Hilo ni wazo zuri,” Alice alisema. “Je, ulisikia hadithi ya Ayitte kutoka mpakani Busia? Alishinda dhuluma za nyumbani na anawasaidia watoto wengine katika jamii yake, nchini Uganda na Kenya.”



Alice alisoma hadithi ya Ayitte darasani. Iliwafurahisha sana hata kengele ilipolia, watoto hawatawanyiki mara moja kama ilivyo kawaida. Walisubiri Alice amalize kusoma, kila mmoja alichukuliwa kimawazo kwa sababu ya simulizi hilo.



## Vitu chanya Vinavyotuzingira

### Watoto wanajitahidi masomoni

Walipofika nyumbani kutoka shuleni, walikaa mezani ili kumaliza kazi zao za nyumbani na kuangalia maelezo katika vitabu vyao. Si rahisi, lakini ni zaidi ya furaha kuwa na kazi za shuleni kufanya tena.

Baadaye jioni hiyo, Zara, Mika, na Susan walikaa mezani, wakicheza fumbo la maneno yaliyohusiana na janga hilo. Zara alikuwa akijaza majibu huku Mika na Susan wakichungulia juu ya mabega yake.

"Ngoma" ni muhimu vipi kwa janga hili?" Susan akauliza, akionyesha neno.

"Ni njia nzuri ya kuwachangamsha watu wakati wa janga hili," Zara akajibu.



"Eee, naam, nakumbuka mama alifurahia mashindano ya densi ya *Jerusalema*," Susan akasema. "Labda tunaweza kuunda mashindano yetu ya densi kwa kutumia ngoma za jadi za Uganda kama *Maganda*, *Ding Ding*, na *Runyege!*" Susan akaongeza.

Zara akaanza wimbo ambao wataucheza wakati wa densi. "Kutambua nguvu za ndoto zangu. Wakati ulimwengu unapotupatia mwema yake, tutasimama juu, wasichana, wavulana inukeni..."

Mika na Susan walianza kubuni mienendo ya densi, na ghafla, watu wazima wakajiunga, kupiga makofi na kurekodi video ya utendaji wao. Walipomaliza kuimba na kucheza, Susan akachukua kipande kirefu cha karatasi ya rangi ya machungwa na kukitandika mezani. Akaanza kuandika.

"Unaandika nini, Susan?" Mika akauliza huku akichungulia juu ya mabega yake akisoma.

Susan aliwaomba wataje visa vizuri vinavyoendelea kote nchini. Janga hili lilikuwa la kutisha, na mambo mengi yalibadilika, lakini pia kulikuwako mambo mengi mazuri yaliyojiri. Bwana na Bi Kego nao walichangia kuongezea kwenye orodha hiyo hadi karatasi hiyo ilipojaa hadithi bora. Watoto hao watatu walibandika karatasi hiyo kwenye ukuta na kupiga picha nazo kwa kutumia simu ya Bwana Kego. Familia nzima ilikuwa na furaha na matumaini walipokwenda kulala usiku huo.

Watoto walikuwa wakifanya kazi zaidi nyumbani na kuanzisha biashara na wazazi wao. Walimu walitoa masomo ya mtandaoni, na mashirika mengine yalitoa vifaa vya kujifunzia kwa watoto ambao hawakuweza kupata mtandao wa intaneti.



## Tumaini la Siku za Mbeleni

### Kuelekeza mawazo kufanya tumaini liwe la kutimika

Siku ya Jumamosi, asubuhi ilikuwa na baridi, na nyasi zilikuwa na umande kutokana na mvua ya usiku. Familia ya Kego ilikaa pamoja sebuleni. Watoto walimwangalia Bwana Kego alipokuwa akipitia kwenye kurasa za nakala ya gazeti la Jumamosi. Kichwa cha ukurasa wa mbele ni habari kuhusu chanjo hio ya KOVID-19.

"Mjomba, unaweza kutuambia zaidi kuhusu chanjo?" Zara akauliza.

"Nilimuona waziri wa afya kwenye televisheni akisema kuwa chanjo hupunguza kusambaa kwa KOVID-19 au kufanya madhara kuwa dhaifu," Mika akasema.



Bwana Kego akakitikisa kichwa kwa makubaliano, "Mika amesema ukweli."

"Basi tunaweza kupewa chanjo, baba?" Susan akauliza. "La hasha, bado." Bwana Kego alitikisha kichwa.

"Serikali inajaribu kupata chanjo zaidi kwa raia, lakini watoto wa umri wa chini ya miaka 12 hawawezi kupata chanjo hiyo," akasema. "Hii ndiyo sababu unapaswa kuwa makini na kuzingatia kanuni za uendeshaji wa kawaida yaani (SOPs) ili uwe salama."

"Watoto, SOPs ni nini?" Bi Kego akauliza.

Wakajibu pamoja, watoto watatu wanaimba, "Nawa mikono yako, vaa barakoa yako, na usimkaribie mwenzio."

"Lakini mjomba, chanjo ni salama?" Zara akauliza, kwa upole huku ameukunja uso wake kwa shauku.

"Ndiyo, Zara," Bwana Kego akajibu. "Wanasayansi waliotengeneza chanjo hizi wamekuwa wakifanya uchunguzi juu ya chanjo kama hizo kwa miaka mingi. Chanjo ni salama."

"Je, umechanjwa, baba?" Mika akauliza.

"Ndiyo," Bwana Kego akajibu.

"Na mama je?" Mika akauliza.

"Bado. Daktari alimshauri asubiri miezi michache baada ya kupata virusi. Hii ni kuhakikisha kuwa chanjo inafanya kazi vizuri."

Bwana Kego akarudi nyuma ya gazeti ambako aliona mazoezi ya watoto.

"Hapa, pata penseli na karatasi. Kuna maswali mengi hapa kuhusu chanjo. Ningependa kuona ikiwa mnajua majibu yake," akasema.

Wakaanza kuandika huku Bwana Kego akisoma maswali. Baada ya maswali kumi, wakayajadili majibu yao.

Zara akamtania Mika, aliyekuwa na majibu saba sahihi kati ya maswali kumi. Susan, dada mdogo, anajua kidogo kuhusu chanjo, lakini Bwana Kego akaahidi kushiriki zaidi watakaporudi nyumbani jioni baada ya kurudi nyumbani kutoka dukani.

Kwa ujuzi huu mpya juu ya chanjo, watoto kwa furaha wakaingia garini kuenda kwenye duka la vitabu. Zara akaruka kweye kiti cha mbele. Susan akaukunja uso kwa sababu Zara amechukua nafasi yake ya kawaida ndani ya gari.

Bwana Kego aliona hasira usoni mwa Susan na akamwambia kwamba katika maisha, mtu hawezi kupata kila anachotaka kila wakati. Watoto wanapaswa kuwa na shukrani kwamba wao huenda shuleni katika gari, ilhali watoto wengine wengi hutembea kwa miguu kuenda shuleni kila siku.



# Nguvu Zetu- Pamoja ni Wenye Nguvu

Kuunda hali ya siku zijazo iwe ambayo tunatara jia kuona

Wiki mpya ilianza kwa msimko mkubwa. Shuleni, Zara na Mika wanajadili wazo lao la kuwasaidia watoto wengine kupata kazi za shule kutoka kwa mwalimu wao. Waliandaa kukusanya vifaa vya masomo kuwapatia watoto ambao hawakuwa na uwezo wa kuvipata.

"Ni wazo zuri sana!" mwalimu Akwi akasema. Aliwahimiza kushirikiana ili kuufanya kisa hicho kuwa mradi wao wa kujifunza shuleni uwe wa sherehe za mwisho wa mwaka. Mwezi uliofuata, watoto walizindua chama kiitwacho "*Let Children of Uganda Learn.*" Watoto walifanya kazi pamoja ili kuendeleza hadithi na kitabu cha hadithi ili kuwasaidia watoto wengine kukabiliana na janga hili. Pia walikusanya vifaa vya kujifunzia na vitabu vilivyotumika kwa usambazaji kwa watoto wote kote nchini. Wengine walianza kutengeneza barakoa kutoka kwa vifaa vya kienyeji.

Sakafu la darasa lilijaa makaratasi. Baada ya masaa mawili ya kazi, watoto walikuwa wachovu lakini walifurahi kwa maendeleo ya mradi wao.

"Kwa kweli, ni vizuri sana. Angalia kile tulichokiunda. Kila kitu kimetoka vizuri," Zara akasema kwa furaha, huku akipiga miayo.




Mika aliinyoosha mikono yake. Ina maumivu kwa ajili ya kukata na kuandika. Watoto walipoanza kufunga na kusafisha, walitambua kiwango kikubwa cha ufanisi wakushirikiana pamoja kwa kutekeleza.

"Hiyo inaitwa roho ya *Ubuntu*, neno la Afrika Kusini. Maana yake ni 'Mimi niko kwa sababu Mpo.' Angalia ni kiasi gani tumefanikiwa kama kikosi," mwalimu Akwi akasema.

"Hilo linaonekana kama neno la Luganda *Obuuntu* sivyo?" Zara akauliza.

Mwalimu Akwi akakubaliana na uchunguzi wa Zara, na akawaambia watoto daima kujua umuhimu wa kushirikiana kwa kufanya kazi pamoja ili kujenga familia na jamii zao.



Watoto walizidi kuchangamka ya sherehe ilivyokaribia. Hatimaye siku hiyo kuu ilipowadia, Zara, Mika na Susan waliamka asubuhi na mapema. Walikuwa na furaha walipoelekea shuleni. Walipakia mizigo na masanduku iliyokuwa na vitabu vya hadithi, barakoa, na vifaa vya masomo katika gari dogo la buluu la Bwana Kego.

Bwana Kego, Mika, Zara, na Susan waliwasilisha masanduku hayo katika shirika la watoto lilipatikana Katwe na Nateete. Watoto walifurahi sana kupokea zawadi hizo na wakacheza na kuimba.

Katika upande mwingine wa mji, Alice na wazazi wake waliwasilisha masanduku huko Nakawa. Abdu na wazazi wake waliwasilisha masanduku kwa watoto huko Kawempe.





Watoto walipofika shuleni ilionekana tofauti. Uiwanja ulijaa magari na boda boda. Mifuko na masanduku vilipakuliwa kutoka kwa magari na bodaboda. Baadhi ya watoto walikuwa wakishughulika na mapambo ya mwisho kwenye hema kwa kuongeza riboni, vyungu, na maua.

Ulikuwa wakati wa furaha kwa watoto. Walijua kwamba kila mmoja wao ana uwezo wa kuleta mabadiliko na mguso unao faa katika jamii.



Kengele ililia na watoto wakakusanyika katika ukumbi mkuu wa wazi kuanza maadhimisho ya siku ya shule. Wazazi, walimu na watoto walitazama maonyesho hayo. Mika ni msimamizi wa ratiba ya sherehe siku hiyo. Aliwakaribisha watazamaji na kutangaza kwamba wametoa vifaa vya kujifunzia kwa watoto elfu saba nchini kote. Watazamaji walipiga makofi na vigelegele kwa kushukuru habari hiyo.

Mika aliita kitendo cha kwanza. Susan akaongoza onyesho la mitindo, akifuatiwa na Zara, Alice, Abu, Justin, na watoto wengine. Watoto walioaonyesha mifano kadhaa ya mitindo ya Uganda na Afrika: mikoba, na vipuipili. Umati ulishangilia watoto walipoonyesha mitindo kadhaa. Ulikuwa wakati wa kuchangamkia daima utakumbukwa.





## Inuka na Uuanguze

### Kupewa zawadi na kutambulika bungeni na kwenye umoja wa mataifa ya ulimwengu

Mradi wa shule "Let Children of Uganda Learn" ulionyeshwa kwenye televisheni, ulitangazwa kwenye redio na magazetini. Zara na Mika walipata mwaliko wa kuwakilisha mradi wao kwenye bunge la Uganda kuwahamasisha watoto wengine kushiriki katika huduma za jamii.

Tarehe 9 Juni, ambayo ni Siku ya Mashujaa nchini Uganda, Zara na Mika walikuwa na mseto wa furaha, na wasiwasi waingia langoni wakikaguliwa na maafisa wa usalama na kupewa vibali vyakuwaruhusu kuingia bungeni. Baada ya uwasilishaji wao, Zara na Mika walishangiliwa. Spika wa Bunge aliwakabidhi medali kwa ushujaa wao na huduma pamoja na mchango wao katika elimu ya watoto. Medali ilikuwa mikufu ya chuma ambayo ilning'inia shingoni mwao kutegemea utepe.



Mwaka mmoja baadaye, Zara na Mika walialikwa kwenye kongamano kuu la Umoja wa Mataifa, lilokuwepo kuanzia mwezi wa Septemba katika Makao Makuu ya Umoja wa Mataifa jijini New York, Marekani.

Kutoka nyumbani kwao Nkumba, watoto hao walikuwa wakizitamani ndege walipozitazama zikitua na kupaa uwanjani Entebbe. Ndoto yake Mika ya maisha ilikuwa kuwa rubani, awe akiendesha na kutua ndege katika uwanja huu.

Usiku kabla ya safari yao, Mika na Zara hawakuweza kulala. Waliwazia safari yao ya kwanza kwa ndege. Siku iliyofuata walifurahi walipopanda ndege pamoja na Bwana Kego baba yao.

Zara alitabasamu wakati alipokuwa akifunga ukanda wake wa kiti. Aliangalia nje kwenye dirisha akiona ziwa Viktoria likifilia ndege ilipo paa angani.



Kwenye kongamano Kuu la Umoja wa Mataifa, umakini wote wa hadhara ulikuwa kwa watoto walio toka Uganda walipowasilisha mbele ya viongozi wa mataifa ya ulimwengu. Kulikuwa na watu wengi ukumbini. Watu wengine walitazama mtandaoni katika nchi zao.

Zara aliwasilisha shairi lililowatia moyo kujijua wao ni nani, wajiamini, wawe na maono makuu maishani pamoja na kuwa na matumaini katika maisha ya mbeleni.

**Inuka uangaze kwa ujasiri  
Yako sauti inahitaji kusikika  
Kwa sababu mbegu za matumaini ziko ndani yake  
Na kwa sauti, utastawi kwa ujasiri  
Changamoto kama ngazi zitakuinua kwenye ufanisi  
Kama jua utainuka  
Katika yote majira utaangaza  
Kwa kuwa hakuna sababu  
Nyota kama wewe hauna majira maalum  
Inuka uangaze  
Kwa uthabiti, kujitahidi, na msimamo.**

Mika kwa ujasiri alianza hotuba yake ya kuhitimisha. "Sisi ni viongozi wa leo. Sisi, watoto wa Afrika, twapaswa kushirikiana kwa kutoa sauti moja. Hebu tuahidi kujitolea kuhudumia jamii zetu tuweze kuzibadilisha. Tusimame kwa uhabiti tulifanye bara letu liwe la kujivunia. Sisi ni kizazi ambacho dunia inatarajia. Kumbuka, "ukitembea peke yako, utatembea haraka. Ukitembea na wengine, utafika mbali". Ni kizazi ambacho ulimwengu umekuwa ukisubiri. Kumbuka, ikiwa unatembea peke yako, unaenda haraka. Ukitembea na wengine, wewe huenda mbali."





## Kuwa na la Kufanya - Ni Juu Yetu

### Watoto wanaahidi kuleta mabadiliko

Kabla warudi kwao, Zara na Mika walikutana na watoto wengine nje ya jengo la Umoja wa Mataifa kupiga picha. Walikumbushana kujihadhari, kunawa mikono, kuvaa barakoa, na kujitenga.

Mika aliwachemsha bongo watoto waliotoka mataifa mbalimbali kulifumbua fumbo hili.

“Kulikuwa na ndege watatu kwenye waya wa umeme; Wawili waliamua kuondoka. Ni wangapi walibaki?”

Watoto walikuwa na majibu na sababu tofauti, lakini jibu rahisi ni hili: Ndege wote walibaki. Ndege hao wawili waliamua kuruka lakini hawakufanya hivyo. Walikuwa na wazo zuri lakini hawakufanya chochote kuhusu wazo hilo.

Somo kuu leo na baadaye ni hili: **Kuwa na cha kufanya!** Usifikiri tu juu yake, fanya! Shiriki katika mabadiliko. Toa sauti yako kila mara. Sauti yako na hadithi yako zinahitajika.

Hatimaye, jiamini siku zote, endelea kuwa na maono, kuwa na mtazamo dhahiri na shirikiana na wengina katika utekelezaji wa jukumu lolote.



“**Ukitembea peke yako, utaenda haraka. Ukitembea na wengine, mnafika mbali.**”

Methali ya kiafrika

TAMATI



## Hadithi za Watoto:

- Matumaini
- Ujasiri
- Shukrani
- Uthabiti
- Kuchua hatua
- Ujasiriamali

## 1 Uthabiti

### Kukumbana na KOVID-19 katika familia

Hannat Namaggala, msichana mwenye umri wa miaka kumi na mmoja kutoka wilaya ya Wakiso alisimmulia ifuatavyo. KOVID-19 imeathiri pakubwa familia ya Hannat, marafiki wengi pamoja na watu katika familia. Mama yake alipoambukizwa na virusi vya korona, watoto walimhudumia. Kwa umri wa miaka 11, alimahimiza dada yakekumshughulikia mama yao. Walipika, walisafisha nyumba na kumpeleka mama yao hospitalini kupata matibabu, mpaka alipoona kabisa.

Hali hii iliifunza familia kushirikiana kwa kufanya kazi pamoja na kuona kuwa kila mmoja aliye karibu nao anafaa. Familia iliendelea kukusanya chakula na kuwapa familia zilizoteseka katika jamii zao. Familia ilijifunza kuweka akiba ya pesa kujitayarishia hali dharura inayoweza kutokea mbeleni.

Ujumbe wake Hannat kwa watoto wengine ni kuwapa tumaini mbeleni. Yeye anajua kwamba kujitolea kuvaa barakoa, kunawa mikono vilevile kujitenga, waliweza kujiinga dhidi ya maambukizi ya virusi vya KOVID-19. Anawahimiza watoto wengine kutilia maanani kanuni za kufuatilia (SOPs) kwa kupapambana na kushinda janga la KOVID-19 warudipo shuleni.

Uthabiti

## 2 Wajasirimali wadogo

Niliamua kuwa mvumbuzi wa ajira

Eryn Kembabazi mwenye umri wa miaka kumi na mmjoja kutoka Kyera katika wilaya ya Mbarara alisimulia haya. Udhhabiti na ubunifu wake Eryn ulimwezesha kupitia katika hali ngumu ya miezi shule zilipokuwa zimefungwa nchini Uganda. Wazazi wake walimfunza kupanda mboga kama aina ya spinachi na pilipili ya kijani. Shangazi yake alimpa vifaranga wa kuku wa wiki nne, kumwanzisha katika safari ya ufugaji wa kuku. Vifaranga hao walipokuwa na kuanza kutaga mayai, aliyauza mayai hayo na kuokoa mapato ya faida yake.

Alipomtembelea bibi yake huko Bushenyi, Eryn alipata fursa ya kujifunza ustadi wa kusuka vikapu, alivyoviuza kwenye soko la jamii. Eryn alipata ujuzi wa kusuka, na akaanza hata kuwafunza jirani zake na marafiki kusuka vikapu. Ilikuwa furaha kugawana ujuzi na watoto wengine katika jamii.

Changamoto kubwa kwake Eryn kukosa kiwango cha elimu chenye maana wakati ambao shule zilikuwa zimefungwa. Kwa kujidhabiti kuendelea na masomo, alihudhuria masomo kwenye runinga na redio kwa sababu hakuweza kupata masomo yaliyokuwa kwenye mtandao kama watoto wengine walivyofanya.

Aliwahimiza watoto wengine kujifunza stadi za kibinadamu na zile zinazowawezesha kuzalisha hela ili waweze kuepukana na upweke. Aliwahimiza hata wazazi kuwanunulia watoto wao vifaa vya kusoma vya kutosha waweze kuvitumia nyumbani kwa ajili ya kuendelea kusoma wakiwa nyumbani.

## 3 Endelea kuamini

Kuuza miwa ili kununua sodo

Kuuza miwa ili kununua sodo. Stella Nekesa mwenye umri miaka kumi na miwili kutokea Kyegegwa alikuwa na kisa hiki cha kueleza. Kabla KOVID-19 ianze, Stella alikuwa akipokea soda kutoka shuleni. Na sasa shule zikiwa kifungoni, hakuweza kupata vifaa hivyo alipopata hedhi. Mama yake alimhimiza kuuza miwakutoka shambani mwao kuwauzia watu wa kambi ya wakambizi ya Kyaka. Hela kutokana na biashara hiyo ndogo ilimwezesha kujinunulia vifaa hivyo na hata kuwanunulia dada zake.

Kwa kuishi kwenye kambi ya wakambizi, Stella alifahamu shida ambazo wasichana wanaweza kukumbana nazo. Aliwahimiza wasichana kujihadhari wakati wa usiku kwa kukaa nyumbani bila kurandaranda, ili wajiepusha na visa vya unajisi.

Ndoto yake Stella ilikuwa kuwa daktari wa watoto ili awatibu watoto walio kambini mwa wakimbizi wasio weza kupata huduma bora za kiafya. Kila siku baada ya kuwasaidia wazazi katika kutekeleza majukumu ya nyumbani, alisoma vitabu vyake kabila giza livamie nyumbani, ambako hawakuwa na umeme. Alikuwa na furaha ya kupindukia shule zilipofunguliwa tena, aendelee na elimu yake.

## 4 Kuchukuwa hatua katika jamii

Kutolea watoto wengine msaada

Kisa cha Rahma Kamulegeya, msichana wa umri wa miaka kumi kutoka Namugogongo Jijini Kampala. Rahma hakujua baraka alizomiliki hadi janga la KOVID-19 lilipotokea. Mwezi Juni mwaka wa 2020, hali ya maisha ilibadilika masomo ya mtandaoni yalipoanza. Nyumbani kwao walikuwa na tarakilishi nne ambazo yeye na ndugu zake wangetumia. Hata hivyo, baadhi ya rafiki zake hawakujiunga kwa masomo hayo ya mtandaoni kwa sababu hawakuweza kupata hela za kulipa karo, kununua tarakilishi na kulipia ada za intaneti. KOVID-19 ilipoanza, alikuwa katika darasa la nne. Sasa hivi anajiunga katika darasa la sita, lakini rafiki zake wengi wangali katika darasa la tano kwa vile hawakuweza kuhudhuria masomo yaliyokuwa mtandaoni.

Ingawa hayuko pamoja na rafiki zake hao, kukaa nyumbani kulimfunza mengi. Alijufunza mambo ya Korani pamoja na mafunzo ya dini ya uislamu, ambayo yalimsaidia kuwa na msimamo dhabiti kidini. Pia amejifunza jinsi ya kusafisha nyumba na anapenda kupika chakula akimsaidia mama yake, anafurahia kutekeleza majukumu ya nyumbani na anaelewa kwamba ni wajibu wao watoto.

Rahma anawajali watoto wengine, familia yake hukusanya vitu vilivyotumika kama vile viatu, nguo na vitabu na kuwapatia watoto hao. Shule inapofunguliwa, ana mpango wa kuwahimiza watoto wengine kuanza kuwatolea wengine vitu ambavyo wao wenyewe hawavitumii.

## 5 Kuwa na msimamo na tumaini

KOVID -19 ilisababisha baba yake kukosa ajira

Joel Jakisa, wa umri wa miaka kumi na mitatu kutoka Tororo. Baba yake Joel alikuwa mwalimu katika shule ya ubinafsi. Shule zilipofungwa, alipoteza ajira yake, na njia pekee ya kupata pesa ilikatika kwa muda wa miaka miwili. Kulikuwa na mabadiliko ya kijamii pamoja na kiuchumi katika familia. Hawakuweza kupata chakula kizuritena kama nyama, samaki na kuku. Kwa hiyo, familia iligeuza mwenendo wake na kuanza kilimo kama njia pekee ya kujinusuru kimapato. Walifanya bidii wakapanda mahindi, mihogo, na soya. Waliyauza mazao hayo.

Wakati shule zilipofungwa, Joel alikuwa anatarajia kufanya mtihani wake wa mwisho wa darasa la saba. Hata hivyo, hakukata tamaa ya elimu yake. Aliendelea kusomea nyumbani, akipitia kwenye daftari zake na akapata gredi ya kwanza kwa alama nane.

Joel ana hofu ya kupata karo yakumwezesha kujiunga katika kidato cha kwanzakuanza masomo yake ya shule ya upili, shule zitakapofunguliwa. Familia imezidi kuweka pesa wanazopata kutokana na kilimo ili waweze kuwarudisha wanao shuleni. Joel anaamini kwamba dhoruba huisha. Msimamo wake dhabiti ni kupata elimu bora aweze kuiletea familia yake fahari.

## 6 Ubunifu huwafanya watoto kuwa na msimamo bora

### Ushairi waleta uwezekano

Mathew Gerald Mugerwa, alitokea Kampala na ni wa umri wa miaka kumi na mmoja. Kama watoto wengi nchini, Mathew alichanyikiwa na mambo janga la KOVID-19, shule zilpofungwa mnamo Machi 2020. Kifungo kilipoanza, Mathew alikata tamaa. Bila marafiki na walimu wake alidhani kwamba ndoto zake zimeangamia.

Shule ndiyo iliyokuwa njia pekee ya kupata maarifa kulingana na fikra zake Mathew. Ingawaje, hata kama shule imefungwa, aliweza kujiamini na kujipa moyo anapoanza mwelekeo mpya wa kukabiliana na hali mpya ya maisha asiyojua. Licha ya athari za janga hili, alichukua hatua njema ya ujasiri alipojitambua kuwa na kipawa cha ushairi, alipozingatia maneno ya umaarufu ya Albert Einstein yanayosema “Dalili halisi ya werevu si maarifa bali fikra”.

Kwa kipindi cha miezi, Mathew aliweza kutunga na kuandika mashairi ishirini akiangazia hofu zake kuhusu ndoto za maisha yake kuhusu siku za mbeleni. Ushairi ukawa sehemu yake takatifu alimojificha kutoka kwa hofu ya vifo vinavyo sababishwa na KOVID-19, hali isiyojulikana inayohusu lini kurudi shuleni sawa na uhaba wa chakula. Mathew amejitahidi kuchangia maelezo kwa maandishi ya Afrika mpya akieleza yale yaliyompata maishani kwa watoto wengine.

## 7 Kulinda imani kwa kusoma

### Kuwa na imani katika hali yoyote

Kisa cha Shalom Efata mwenye umri wa miaka kumi na miwili kutoka Masaka. Katika wakati wa kifungo, Shalom aligundua kwamba anapenda kusoma. Kupenda kusoma vitabu kulimsaidia kupata ushindi dhidi ya hali ya upweke na hali isiyoeleweka ya kutokuwa shuleni. Mama yake alimpatia vitabu mbalimbali, kama vile “Rich Dad, Poor Dad”, kilichoandikwa na Robert Kiyosaki na Sharon Leichter. Kitabu hiki kilimpa moyo wa kuzindua miradi akiwa angali wa umri mdogo. Wazazi wake na marafiki walipompa pesa kama zawadi kwa kuhitimu vyema mtihani wake wa darasa la saba, alianzisha biashara ndogo.

Shalom alikuwa ameshasoma kitabu cha Peter Abesiga kinachojulikana kama “Adopt or Die”, kilichomtia moyo kuweka barabara malengo yake ya elimu na kazi angefanya baada ya kuhitimu masomoni. Hatimaye, alikuwa na uhakika wa kushindwa kwa kujifunza kuendelea kwa kurekebisha makosa yake. Katika muda wote wa kifungo, alijielewa vyema kuweza kuwapata stadi na mawazo yanayofaa maishani. Katika hali hii ya mabadiliko, ujumbe wake kwa watoto wengine ni kwamba waweze kuwa na cha kufanya kinachoweza kuwasaidia katika kila hali ya maisha na katika kila hali wamtegemee Mungu anayewatolea watu wote hekima.





## Safari ya Ukalimani

### Ukulima na kujifunza lunga mpya

Mwendo wa ujasimali. Ukulima na kujifunza lugha mbalimbali, Esther Elizabeth Bugosera mwenye umri wa miaka kumi vile alivyosimulia kutoka wilaya ya Kapchorwa. Esther alikuwa katika hali ya upweke na uzembe katika siku za kwanza za kifungo kwa vile hakuwa na kazi nyingi za kufanya huko nyumbani Mukono. Kwa hiyo, aliamua kuenda kuishi na mama yake katika chuo cha uwalimu cha Kapchorwa, alikokuwa akifanya kazi, Uganda Mashariki.

Esther alianza kilimo cha mseto nyuma ya nyumba yao katika ardhi yenye rutuba huko Kapchorwa. Alijifunza kulima, kupanda mimea kama kabeji, nyanya, ndizi, viazi vya kizungu, mahindi na vitunguu. Alijifunza pia kuchunga wanyama kama ng'ombe, mbuzi na batamzinga. Pia alipata ushujaa wa kukama ng'ombe halafu akaanza kuuza maziwa.

Kwa tabia yake ya hamu ya kutaka kufahamu mambo na ubunifu, Esther alijifunza kuzungumza lugha mbili zinazozungumzwa katika jamii hiyo. Aliweza kuzungumza Kupsabiny na Kiswahili. Alipendelea pia utalii wa kienyeji na aliweza kutembelea kijito cha "Sipi falls" na mapango.

Kuzuru huku kulimfanya aweze kuthamini vitu vinavyopatikana katika mazingira ya jamii iliyokaribu naye. Ingawa hakuwa na tarakilishi na alikumbana na changamoto za mtandao, alijidhabiti kuendelea kwenye mtandao kwa kutumia simu ya mkononi ya mama yake, aliyokuwa akiitumia pamoja na kaka yake.



## Shughuli katika jamii

### Kurudi Shuleni ni upendeleo kwa watoto wakimbizi

Mariam Ukuna mwenye umri wa miaka kumi na miwili alisimulia kwamba ilikuwa bahati Kurudi shuleni tena kwa watoto katika kambi ya wakimbizi. Alisimulia kutoka Kyegegwa. Mariam ni mkimbizi kutoka Kongo na aliishi na wazazi wake, kaka zake na dada zake katika kambi ya wakimbizi huko Kyaka nchini Uganda. Tangu shule zilipofungwa mnamo mwezi wa Machi mwaka wa 2020, maisha yake hayakubadilika. Watoto kwenye kambi za wakimbizi walitegemea walimu kuwashauri na kuwakuza. Alikosa kupata sabuni na sodo, vifaa alivyokuwa akipokea shuleni. Ingawa hakuwa shuleni na alikuwa akiwazuru jamaa zake mitaani, alibaki jasiri.

Mmoja wa wanafunzi wenzake aliambukizwa na virusi vya COVID-19, hali hii ilimfanya Mariam kuelewa kanuni za kujikinga. Alisalia wanyumbani wakati wote na alipotumwa dukani na wazazi wake, alivaa barakoa na kujitenga. Aliporudi nyumbani, alinawa mikono yake barabara. Aliwahimiza ndugu zake na wazazi kujilinda.

Muda aliokaa nyumbani ulimfanye athamini na kutekeleza majukumu ya nyumbani. Alifagia nyumba, uani na kuwatunza wadogo wake. Pia alijifunza kusuka vikapu, vilivyotumika nyumbani na aliamua kukuza ustadi wake kuweza kusuka vikapu vya kuwauzia wakimbizi kambini. Mariam aliwapa moyo rafiki zake kuendelea na masomo wakitumia vitabu vilioko karibu na warudi shuleni zitakapofunguliwa.

## 10 Shukrani na ustahimilivu

### Wazazi walipoteza ajira lakini familia ikaunganika

Wazazi walipoteza ajira zao lakini familia ilikaa kwa pamoja, Immaculate Oyella mwenye umri wa miaka kumi na miwili alivyosimulia kutoka Gulu. Hali ya maisha ilikuwa ngumu tangu kifungo cha kwanza mnamo mwezi wa Machi 2020. Mama yake Mary alikuwa mwalimu katika shule ya upili ya Pope Paul IV Anaka katika wilaya ya Nwoya. Mama na baba yake walipopoteza ajira, hali ilibadilika na kuwaendea mrama. Baba yake alifungua duka dogo mjini Gulu ili limsaidie kupatia familia yake riziki.

Mary alikaa nyumbani na mama yake, alikojifunzia kulima kusafisha nyumba na kupika vyakula vya Kicholi. Kukaa na mama yake kulifanya kuwa msichana anayewajibika. Mary na dada zake wawili waliweza kuunda mfereji wa maji kwa kutumia vifaa vya plastiki, kibuyu cha uzito wa lita tano na chupa ya maji ya plastiki. Familia ilizidi kunawa mikono wakitumia sabuni kupambana na maradhi ya korona. Ubunifu huu uliweka mfano bora kwa familia nyingi kijijini na wakaweza kuwa na sehemu za kunawia mikono katika makao yao kwa kutumia vifaa vya kienyeji kujilinda na kutunza usafi.

Ingawa Mary alikuwa angali katika darasa la tatu, darasa alimosalia kumaliza miaka miwili, alikuwa mchangamfu aliporudi shuleni. Familia yake ilibaki na imani na udhabiti.

Shukrani

## 11 Kufanya hela ni hali ya kupewa moyo

### Kujifunza stadi mpya kufanya hela

Daniela Owomuhendo wa umri wa miaka kumi na mitatu kutoka Kampala alitoa kisa chake. COVID-19 iliwafunza watoto masomo mengi na kuwapa ufahamu vile jamii ilivyoathirwa nchini mwao. Walisikia visa vya wasichana wakiozwa wakiwa wangali wadogo ama kunajisiwa na kuwa akina mama wachanga.

Daniela alikuwa mmoja wa wasichana wachache nchini Uganda ambao wazaziwao walikuwa na uwezo wa kununua tarakilishi ili waweze kutumia katika masomo wakiwa nyumbani kwa mtandao. Katika kifungo, alijifunza stadi kadhaa za kupata pesa kwa kuunda mkeka ya kutumiwa milangoni na kwenye malazi. Alianza pia kutengeneza vyakula kamavitumbua, mandazi na sambusa, vitu ambavyo mama yake alimsaidia kwa kuviuza kwenye saluni yake. Aliweza kuhifadhi mapato yake ndani ya kisanduku chake. Daniela ana ndoto ya kuanzisha upishi wa mikate kwa nia ya kufanya pesa nyingi.

Daniela ana mawazo ya ubunifu. Ameandika nyaraka kwenye majarida ya watoto ya "Rainbow" na TOTO kuwafunza watoto jinsi ya kuzuia COVID-19. Alikuwa na furaha kwa kuleta mabadiliko nchini mwake kupitia mamilioni ya watoto walio rejelewa na majarida hayo.

KUTIA MOYO



# Shughuli, Michezo, Wimbo na Shairi

Shughuli hizi zitakusaidia kuelewa na kukumbuka habari muhimu kuhusu COVID-19. Unaweza kufanya mazoezi peke yako au na watoto wengine kujifunza zaidi. Kumbuka kuziandika chini.

“ Wino dhaifu zaidi ni bora kuliko kumbukumbu yenye nguvu zaidi. ”  
*Mithali ya Kichina*



## Shughuli ya kwanza: Mto wa Uhai – Kila Dhoruba Hupita

Shughuli hii iliwasaidia watoto kurejelea yale yaliyopita ili waweze kuangazi visa bora vilivyotokea. Ni jambo la busara kuwasaidia watoto kutoangalia changamoto bali kuzingatia yale mema waliyojifunza.

### Maagizo kwa walimu:

- Waongoze watoto katika maswali haya matatu, wahimizi kuwa wenye ukweli na wenye mawazo ya kushirikiana.
- Watoto wanaweza kutumia maneno, picha, nyimbo au mashairi kujiasilisha.
- Wahimize kujadiliana pamoja majibu yao wakiona kwamba ni vizuri kufanya hivyo.

**Vifaa vinavyohitajika ni:** Kalamu, penseli, vifaa kama maka, karatasi ama kitabu.



### Maswali:

1. Kwa kuangazia hadithi ya Zara na Mika, ni dhoruba gani uliyopitia katika mwaka mmoja au miwili iliyopita hususan wakati huo wakutokuwa shuleni?
2. Uliwezaje kufaulu changamoto ulizopitia?
3. Ni mafunzo gani uliyoweza kupata kutokana na maisha yako, familia na jamii?



## Shughuli ya pili: Pongezi na Maandiko

Shughuli hii iliwasaidia watoto kuangazia mema waliyo naye kwenye familia na jamii zao. Watoto walijifunza pia stadi za kuandika – wakiandika fikra na mawazo yao. Kuandika mambo kuliweza kuweka fikra zao huru kutokana na mawazo maovu, na kwa wakati mmoja huo kuwaongezea nguvu katika mawazo yao na ndoto zao. Walipopata uzoefu wa ustadi wa kuandika maombo yanaliyowapendeza, mawazo yao yalielekea kwenye ubora uliokuwa karibu nao, basi kuangalia uwezekano wao siku za mbele.

### Maagizo kwa walimu:

- Waulize watoto wachukue muda wafikirie juu ya vitu kumi wanavyopongeza.
- Waviandike chini kwenye daftari zao. Watoto wahimizwe kufanya shughuli hii kila jioni kabla ya kuenda kulala.
- Siku itakayofuati, waweze kushirikiana katika kujadili pongezi zao na wenzao kuona kama mambo yao ni sawa.
- Mwalimu awaongoze watoto kuunda orodha ya darasa kuhusu mambo wanavyopongeza. Wanafunzi wasome orodha hiyo kila asubuhi kama desturi kabla ya kuanza kwa shughuli nyingine darasani.



## Shughuli ya tatu: Mimi ni nani?

Shughuli hii iliwawezesha watoto kuyagundua maneno bora waliyoweza kutumia vile walivyoweza kujieleza wenyewe. Watoto walipofanya hivyo kila wakati, kila siku fikra zao zilihama, wakajipatia udhabiti kujielewa wao ni nani, bali haikuwa vile watu wengine walivyoona au kuwaambia kuwahusu.

### Maagizo:

- Kila asubuhi, mtoto alijiangalia kiooni na kujiuliza mwenyewe, "Mimi ni nani?" na ikiwa hawakuwa na kioo, walijichukua kama waliokuwa wakijitazama kwenye kioo. Juu ya hayo, watoto walipaswa kukumbuka kutumia maneno bora kujieleza.
- Mwalimu aliwahimiza kurejelea jinsi Mika na rafiki zake walivyojiamini katika hadithi ya je, "mimi ni nani?" kwa kujidhabiti.



## Shughuli ya nne: Mchezo wa Kurukaruka kwa Tumaini

Mchezo huu uliwasaidia watoto kuwa na ndoto za ajabu, kuwa na malengo na kuwapa matumaini ya siku zijazo. Hii ndio maana uliitwa mchezo wa kurukaruka kwa tumaini.

### Maagizo:

- Watoto walitakiwa wachore michora ya visanduku ardhini wakitumia chaki au kipande cha kaa na waanze kucheza mchezo wa kurukaruka kwa tumaini. Kila mtoto alipaswa aruke mara tano kwa mguu mmoja, na kutua kwa miguu miwili. Walipotua, walitaja walichopendelea kuwa maishani wakuwapo watu wazima, na kutoa sababu kwa nini. Waliambiwa wasikike kwa uhakika na kwa furaha.

Tazama mifano hii:

Ruka, ruka, ruka, ruka, ruka, mimi ni daktari, na nitaokoa maisha ya watu.

Ruka, ruka, ruka, ruka, ruka, mimi ni mwanahabari, nitasambaza habari bora.

Ruka, ruka, ruka, ruka, ruka, mimi ni rubani, na nitawapeleka watu sehemu mbalimbali.

Ruka, ruka, ruka, ruka, ruka. Mimi ni mama, na nitawalea watoto wa ajabu.

Ruka, ruka, ruka, ruka, ruka. Mimi ni afisa wa polisi, nitatunza sheria na usalama.

Ruka, ruka, ruka, ruka, ruka, mim ni Mwanauganda halisi msanii wa mitindo. Nitaendeleza utamaduni wa kiafrika duniani.



## Shughuli ya tano: Upekuzi wa Maneno

Shughuli hii iliwasaidia watoto maneno mengi kuhusu COVID-19. Hii ilikuwa njia ya ajabu ya kuipanua misamiati yao na hamu ya kujifunza mengi.

**Maagizo:** Watoto waliweza kupitia kwa upekuzi wa maneno wakitafuta maneno 15-20 yanayohusiana na COVID-19. Pengine maneno hayo yalikuwa ni ya kawaida kwa watu kwa kinga na kutibu virusi ama waliyokuwa wakitumia kujaribu kushikana na hali.





## Shughuli ya sita: Matendo Bora

Watoto walipitia mambo mengi mbalimbali maishani mwao na hata katika jamii. Shughuli hii iliawezesha watoto kuwazia mambo bora yaliyowazingira. Orodha iliopo chini hapa iliakilisha baadhi ya mambo bora yaliyofanyika kwenye familia zetu na taifa licha ya athari za virusi.

**Maagizo:** Isome orodha uweze kutoa mambo kumi uliyoona au uliyosikia katika familia yako au jamii. Watoto wawe na ufasaha na wawaze kwa upana kuhusu mambo bora.

### Matendo Bora

#### 1 Udhabiti

Watoto walikuwa watendaji nyumbani na hata kwenye jamii zao.

#### 2 Ujasirimali

Watoto na wazazi walitangeza maji yakunyunyizia kuangamiza virusi pamoja na barakoa. Wengine walitembeza bidhaa na kuviuzia watu nyumbani kutoka sokoni, madukani, supamaketi, mikahawani na maduka ya madawa.

#### 3 Masomo

Walimu walitoa mafunzo kupitia mtandaoni na vifaa vingine vya mawasiliano. Mashirika ya ubinafsi yaliweza kusambaza vifaa vya masomo kwa jamii ambazo hazikuwa na mtandao.

#### 4 Kijamii

Familia zilikuwa na muda wa kuwa pamoja wa kutosha. Watu wengi walifanya mazoezi ya kimwili ili kuiboresha miili yao. Wengine walifahamu umuhimu wa kula matunda na mboga.

#### 5 Mitandao ya kijamii

Watu walibadilishana ujumbe wakuhimizana wakitumia mitandao ya kijamii, na hata kuzungumza kuhusu afya ya mawazo na kutoleana sala.

#### 6 Elimu

Watoto walisoma kwa bidii kujaribu kuukomboza muda uliopotezwa ili waweze kupita mitihani yao vyema.



## Shughuli ya saba: Maswali na Majibu juu ya Chanjo za KOVID-19

Kuna kutatanishwa na kutoelewa vyema kuhusu chanjo dhidi ya KOVID-19. Shughuli hii iliwapa watoto habari halisi kuhusiana na chanjo. Hii ilikuwa habari ya kuaminika Kituo cha Afrika cha kuinga na kuzuia maradhi (African Centres for Disease Control and Prevention).

### Maagizo:

- Mwalimu aliwaambia watoto wachukue karatasi na kalamu waandike habari hii ya muhimu juu ya chanjo na kuchanja nchini Uganda. Watoto walipaswa kushirikiana kujadili juu ya habari hii na familia zao pamoja na marafiki zao kuweza kufamu vyema.

### Swali la kwanza: Chanjo zinatumiakaje?

**Jibu la kwanza:** Chanjo hutumika kwa kuufanya mwili kudhani umeambukizwa na virusi, basi kuushtua uzindue kinga yake wenyewe kupambana na kirusi.

### Swali la pili: Je, chanjo ni salama?

**Jibu la pili:** Chanjo ni salama, hazina athari mbaya, zinakinga watu dhidi ya virusi vya KOVID-19. Ila, zinawaza kuleta dalili za homa, maumivu ya misuli na kichwa na uchovu, lakini ni vya kipindi kidogo.

### Swali la tatu: Ni watu gani wanaopaswa kupata chanjo kwanza?

**Jibu la tatu:** Wahudumu wa afya, ndio wa kwanza kuingwa ili kuzuia kusambazwa kwa ugonjwa huu kwa wagonjwa wao. Wengine ni wazee na wale wenye magonjwa kama kisukari. Na pia wengine wanaotumikia umma kama walimu, wafanyakazi wa viwandani na wafanyakazi wa benki.

**Swali la nne: Je, chanjo zinapatikana kote nchini?**

**Jibu la nne:** Chanjo zipo kila mahali nchini, bali, kwa vile vipimo vyake havitoshi, kila mtu hatachanjwa hivi. Lengo ni kutoa vipimo vyakutosha kwa kila mmoja anayehitaji.

**Swali la tano: Ninaweza kukoma kuvaa barakoa baada ya kupata chanjo?**

**Jibu la tano:** Hakuna habari kamili kuhusu ni lini ndio salamawatu wangeacha kuvaa barakoa. Kuna uwezekano kwamba watu waliochanjwa watakingwa kutoathirika vibaya na ugonjwa, lakini wanaweza kuambukizwa na kuwaambukiza wengine. Ni bora kuvaa barakoa ukiwa katika umma pamoja na kujitenga ukizingatia kanuni zingine za kujikinga.

Ukitaka kujua mengi zaidi tafadhali tembelea <http://africacdc.org/download/questions-and-answers-on-covid-19-vaccine/>



## Shughuli ya nane: Kushirikiana katika Kupiga Makofi

Shughuli hii itawafunza watoto kuthamini kushirikiana pamoja kwa kufanya kazi ili kupata matokeo mema.

### Maagizo:

- Mwalimu anawaomba watoto takriban watoto kumi kusimama juu. Kwanza wote wanapiga makofi kwa pamoja, wakitumia kidole kimoja, halafu viwili.
- Watoto waangalie vile hao watoto kumi walivyopiga makofi kwa pamoja, lakini sauti hafifu. Sauti ilizidi kuvuma idadi ya vidole ilivyo zidi kuongezeka.





## Shughuli ya tisa: Shairi

Shughuli itawasaidia watoto kutumia maneno bora katika utumbuizaji.

### Maagizo:

- Mwalimu atawagawanya watoto katika makundi na kuwaomba wajitokeze kusoma shairi. Mwanafunzi akariri peke yake au na wenzake na waweze kukariri kwa kushindana kwa mazingira yao waone nani ndiye bora. Ilionekana kama mchezo huku wakijifunza.

### INUKA NA UANGAZE

Ninainuka na kuangaza

Kama jua

Ninainuka na kuangaza na kujiamini mwenyewe kwa kuwa hiyo ndiyo utajiri wa kweli.

Wakati nyakati zinabadilika na mambo yanazidi kuwa magumu

Ninashikilia mkono na kushiriki nuru yangu

Kama jua

Ninainuka na kuangaza.

Ninainuka na kuangaza kwa ujasiri,

Wakati sauti yangu inapaswa kusikilizwa

Kwa mbegu za matumaini ziko ndani yake

Ndani yake nitanawiri kwa ujasiri

Kutazama changamoto kama hatua rahisi kuelekea ukuaji.

Nitainuka kama jua

Nitaangaza kwa misimu yote

Kwa sababu hakuna sababu, hakuna msimu

Kwa nyota maalum kama mimi

Ninaangaza kuelekea ndoto zangu

Chukua jukumu la hatima yangu

Tumia nguvu ya ndoto zangu kuangaza mishumaa mingi

Nitakuwa bora zaidi kwa chochote ninachofanya

Acha nyayo zangu popote nitakapokwenda.

Ninainuka na kuangaza

Kwa uthabiti, ulabibu, ujasiri

Kwa faraja ya matumaini na mafanikio

Itaniweka kwenye motisha

Daima kufanya kile ambacho ni sahihi na cha kweli

Kwangu

Na wale ninaowajali

Wale ninaowasimamia.

Ninainuka na kuangaza

Pamoja na familia yangu na jamii

Kwa umbali wa furthest ni kufunikwa

Kutembea pamoja

Ninapenda kufanya kazi pamoja

Kutembea njia ya mshindi.

Ninang'a ili kuleta mabadiliko

Kuunda hadithi mpya za Kiafrika

Kwa historia na hadithi za watoto wa Kiafrika

Ninang'a ili kuleta mabadiliko

Kuwa mtu wa heshima na uadilifu

Kulifanya jukumu langu la kuifanya dunia hii kuwa mahali bora pa kuishi

Kizazi hiki

Na kijacho

Ninainuka na kuangaza.

INUKA na

U





## Shughuli ya kumi: Ahadi na Kujitolea

Shughuli hii iliwafunza watoto kujiahidi kuhama kutoka kwa nafsi zao kuleta mabadiliko katika jamii zao.

### Maagizo:

- Mwalimu aliwaongoza watoto kufanya orodha ya vitu vitatu walivyojitolea kufanya wenyewe, katika familia zao na jamii, walivyowatumikia wengine miezi mitatu iliyopita. Watoto walijadili kujitoa kwao na wenzao, wazazi na walimu kuwasaidia kuendelea na kujitoa huko. Mwishoni mwa kila mwezi, mwalimu aliwaomba watoto kujadili kuendelea kwao kuwatangaza watoto walio chukua hatua halisi ya kujiahidi kumaliza kipindi cha miezi mitatu.

Mfano wa kujiahidi:

Ninajiahidi kusoma kitabu cha kunipa motisha kila siku kumaliza miezi mitatu.

Mimi ..... ninajiahidi ku .....



## Shughuli ya kumi na moja: Maneno mapya na Kuangazia Maswali

### Maagizo:

- Baada ya kusoma kitabu cha hadithi, watoto walijibu maswali yafuatayo.



- Ni maneno gani mapya uliyojifunza kutokana na hadithi hii?
- Zara na Mika walifanya nini kuinuka na kuangaza?
- Nani mwingine aliyetajwa hadithini?
- Ni nani mhusika wako mashuhuri na kwa nini ni mashuhuri kwako?
- Ni vitu gani vitatu ulivyojifunza kutokana na hadithi hii?
- Kwa kusoma hadithi kwa sauti, ni sehemu zipi za kitabu zinazohusiana na maisha yako?



## Shughuli ya kumi na mbili: Wimbo

### Maagizo:

- Soma na usikilize wimbo huu na ujifunze.
- Imba kila siku kuinua hali yako kutawala juu ya hofu zako ili uwe na maono makuu. Unaweza kuimba peke yako au na wengine.
- Andaa mashindano ya kuimba katika jumua yako ili uone ni nani ndiye bora kuliko wengine.
- Ufanye kuwa mzaha ukijifunza.

### Wimbo wa Nyota unaochipukia: Nguvu ya ndoto

#### Kiitikio:

Mimi ni nyota inayochipuka, mimi si wa kawaida  
Naota ndio naota, ninaota kwa sababu mimi ni nyota inayochipuka  
Nina ujasiri... kukumbatia hofu zangu  
Ninafikia... Kwa nyota  
Kutambua nguvu ya ndoto zangu, nguvu ya ndoto zangu.

#### Mstari:

Tukiamini, tunaweza kutimiza,  
Kugundua maana ya, kuishi huru na kuinuka  
Zaidi ya kile tulichoota ndani,  
Ndani ya kila moyo, kuna cheche ya miujiza  
iangazayo mawazo yako kuyabadilishakuwa makuu,  
Kubadilika kuwa makuu  
Kutambua nguvu ya ndoto, nguvu ya ndoto.

#### Kiitikio:

Mimi ni nyota inayochipuka, mimi si wa kawaida  
Naota ndio naota, ninaota kwa sababu mimi ni nyota inayochipuka  
Nina ujasiri wa kukumbatia hofu yangu  
Ninafikia... Kwa nyota  
Kutambua nguvu ya ndoto zangu.

#### Mstari:

Wakati dunia inavyotupa bora zaidi,  
Tutasimama juu  
Wasichana, wavulana, Inukeni  
Nyinyi ni kizazi... Dunia imekuwa ikisubiri  
Ulimwengu hautakuwa kama kawaida  
Kuna uwezo kwenye ndoto x2

#### Kiitikio:

Mimi ni nyota inayochipuka; mimi si wa kawaida  
Naota ndio naota, ninaota kwa sababu mimi ni nyota inayochipuka  
Nina ujasiri... kukumbatia hofu zangu  
Ninafikia... Kwa nyota  
Kutimiza nguvu ya ndoto zangu, nguvu ya ndoto zangu.

Mimi ni nyota inayochipuka, mimi si wa kawaida  
Naota ndio naota, ninaota kwa sababu mimi ni nyota inayochipuka  
Nina ujasiri... kukumbatia hofu zangu  
Ninafikia... Kwa nyota  
Kutimiza uwezo wa ndoto zangu, nguvu ya ndoto zangu.



## Shughuli ya kumi na tatu: Angazia na Ujifunze

### Maagizo:

- Mwalimu aliwaongoza watoto kusoma hadithi nyingine za watoto. Kila hadithi ilikuwa na somo la kujifunza. Watoto wazingatie hadithi na wjadiliane mafunzo waliyojifunza kutokana na hadithi.
- Mwalimu aliwaongoza watoto katika maswali haya manne:



1. Ni hadithi ipi unayohusika nayo na kwa nini?
2. Unajifunza nini kutokana na hadithi hizi?
3. Ni ujuzi gani ambao watoto hao walitumia?
4. Je, unaweza kufanyaje kuyatawala maisha yako na kutumikia familia yako ama jumua?

# #Nijuuyetusisi

# Zara & Mika

## Kuongoza Mabadiliko Chanya Katika Jamii Zao

Sauti ya watoto ni kitabu kinachojumisha hadithi kutoka kwa watoto wakijadiliana maoni yao na hayo waliyoyapitia katika kipindi cha janga la KOVID-19. Kitabu hiki kinatoa vifaa maalum vinavyo wasaidia watoto kustawi, kubuni, kuiga na kusoma kuendeleza stadi za kijamii na kimoyo zinazoweza kudumu kwa maisha.

Kitabu hiki kinawapa watoto fursa ya kufurahia na kujifunza kutoka kwa visa vya watoto wengine vya udhabiti, ustahilivu, kuwa na tumaini na kuwa na ujuzi wa kibiashara. Kitabu hiki ni cha uhusiano, uwakilishi na uangazaji wa hali halisi ya maisha ya watoto. Visa vinaambatana na tamaduni vikiangazia watoto walio katika jamii duni kama wahusika wakuu. Kitabu kinawasaidia watoto kusoma kupata mwanya wa kujifunza, kuwahimiza kubaki shuleni na kuwa shupavu katika kusoma baadaye masomoni.

Sauti ya watoto hutoa vifaa vya utendaji kujenga ustahimilivu kuwawezesha watoto kufaulu na kustawi. Kitabu kinajumisha miradi iliyoegemea kwa vitendo vya kusoma vinavyo weza kuwafanya watoto kupata mawazo ya kuweza kupata suluhisho ya hali tata ya maisha shuleni na hata nyumbani. Yaliyomo huwapa watoto nafasi ya kujielewa, kuelewa jamii, ushirika wa kijamii na mabadiliko ya kijamii.

Sauti ya watoto inamiliki tumaini, na sauti za imani ambazo watoto wetu wana hamu kuzisikia. Methali ya kiafrika inasema " ukienda peke yako, utaenda kwa kasi, ukiandamana na mwenzako, mnaifika mbali", huwagusa watoto wengi waweze kutenda shughuli pamoja. Watoto wa Uganda wanatenda mambo ya huruma na kwa ushirikiano, hali ya kijamii inayohitajika katika dunia hii.

— **GERALDINE LAYBOURNE**, Mteteaji wa watoto na aliyekuwa rais wa Nickelodeon

"Ni furaha ya ajabu kusoma hadithi halisi zinazotolewa na watoto kuhusu maisha yao na mambo yanayohusu enzi hizi za sasa. Somo kuu la watoto katika Afrika Mashariki na duniani nzima. Tunahitaji vitabu kama hivi kukitia mori kizazi cha sasa na hata kijacho."

— **NISHA LIGON**, Kiongozi mkuu wa uchapishaji wa Akili and Me pamoja na Ubongo Kids



ISBN 978-9913-9930-0-5



9 789913 993005